

## **SEMINA KWA WAZALISHAJI, WAAGIZAJI, WASAMBAZAJI NA WAUZAJI WA BIDHAA ZA UMEME NURU**

Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kwa kushirikiana na taasisi inayoshughulikia masuala ya fedha (IFC) limeandaa semina kwa wadau wote wa umeme nuru itayowahusisha wazalishaji, waagizaji, wasambazaji na wauzaji wa bidhaa za umeme nuru. Semina hiyo itafanyika tarehe 2018-03-21 kuanzia saa tatu (03.00) asubuhi mpaka saa saba (07.00) kamili mchana katika ofisi za **TBS** Makao Makuu zilizopo Ubungo jijini Dar es Salaam.

Katika Semina hiyo elimu kuhusu utekelezaji wa viwango vya bidhaa husika kama ilivyoainishwa katika viwango vya lazima vya kitaifa **TZS 1951:2017** na **TZS 1952 - 9-5:2017** itatolewa, ili waagizaji, wasambazaji na wauzaji wa bidhaa za umeme nuru waweze kufuata na kutekeleza matakwa ya lazima ya viwango husika.

Washiriki wanatakiwa kujiorodhesha majina yao kwenye Ofisi za TBS Makao makuu, zilizopo Ubungo na ofisi za TBS zilizopo jengo la Diplomat, mtaa wa Kaluta/Mkwepu Posta. Mwisho wa kujiandikisha ni Jumatano tarehe **2018-03-16** saa kumi kamili (10) jioni.

Zingatia kuwa watakojiandikisha ndio watakaoshiriki katika semina hiyo.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:

**Mkurugenzi mkuu**

**Shirika la Viwango Tanzania (TBS)**

**S.L.P 9524**

**Dar es Salaam**

**Simu: +255(022)2450206**

**Hotline: +0800110827**

Barua pepe: [info@tbs.go.tz](mailto:info@tbs.go.tz)

au

**Meneja Mradi,**

**Lighting Africa/Tanzania,**

**Mtaa wa 50 Mirambo**

**P. O. Box 2054,**

**Dar es Salaam.**

**Simu: +255-22-216-3246**

